

# TANGAZO LA KAZI

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO ANAWATANGAZIA WANANCHI WA WILAYA YA LUSHOTO NAFASI YA KAZI YA MUDA YA KUKUSANYA MAPATO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO.**

*Kwa tangazo hili waombaji wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hizi kama ilivyoainishwa katika tangazo hili wanakaribishwa kutuma maombi yao.*

**IDADI YA NAFASI:- ISHIRINI NA MBILI (22).**

**MAJUKUMU:-**

- i. Kukusanya ushuru katika eneo utakalopangiwa na mwajiri
- ii. Kuhakikisha mapato yote ya Halmashauri yanakusanywa kwa kufuata taratibu
- iii. Kuhakikisha matumizi sahihi ya mashine ya kukusanyia mapato (POS)
- iv. Kuwasilisha fedha yote inayokusanywa katika eneo husika na kwa wakati.

**SIFA ZA MWOMBAJI:-**

- i. Awe ni mkazi wa Wilaya ya Lushoto
- ii. Awe ni kitambulisho cha NIDA
- iii. Awe na Afya njema mwaminifu na mwenye kujituma
- iv. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45

- v. Asiwe amepatikana na kosa lolote la jinai
- vi. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne (iv)
- vii. Mwombaji aambatishe wasifu (CV) na nakala za vyeti vya taaluma pamoja na cheti cha kuzaliwa
- viii. Awe na uelewa wa masuala ya fedha
- ix. Watakaochaguliwa wataarifiwa tarehe ya usaili

Barua za maombi ziwe zimefika katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji si zaidi ya tarehe 17/02/2023. Saa tisa na nusu mchana.

Maombi yatumwe kwa:-  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto  
S.L.P. 32,  
Lushoto - Tanga.

**Limetolewa Na.**  
**Mkurugenzi Mtendaji,**  
**Halmashauri Ya Wilaya Lushoto**



.....  
**ELIEZER MOSES**

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**LUSHOTO**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**LUSHOTO**